Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# ELIMU Bulletin

JARIDA LA MTANDAONI: Toleo Na.44, - 2025

wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ

*Tunaboresha Elimu Yetu*






# WALIMU NI MSINGI WA MAENDELEO YA TAIFA

## - MHE. MAJALIWA

## - KAZI IENDELEE -

# TAHARIRI

## SAMIA SCHOLARSHIP EXTENDED DS/AI+ KUANDAA MABINGWA WA DATA NA AKILI UNDE

Katika karne ya 21 inayotawaliwa na sayansi na teknolojia, mataifa yote duniani yanapiga hatua mbalimbali kwenda sambamba na mabadiliko haya. Tanzania imeendelea kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha haiachwi nyuma. Kupitia Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023, Serikali imeweka mkazo katika kukuza elimu ya fani za kimkakati ambayo ni pamoja na sayansi na teknolojia, kwa lengo la kuondoa pengo la wataalam katika nyan ja hizo watakaowezesha na kuchochea maendeleo ya taifa.

Moja ya kimkakati upande wa elīmu ni kuhakisha Sayansi na teknolojia inapewa kipaumbele katīka ujifunza ji na ufundīsha ji kwa ngazi zote, kipekee elimu ya juu, dhamira ya Serikali imeonekana wazi kupitia uanzishwa ji wa mpango wa Ufadhili wa masomo ujulikanao kama Samia Skolashipu ambayo ina matawi matatu, Samia Skolaship, Skolaship Extended na Samia Skolashipu Extended PS/AI+.

Kupitia kurasa hizi za elimu bulletin leo tuangazie Samia Scholarship extended PS/AI+. Tuanze kwa kutoa Kongole kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Awamu ya Sita, kwa kubuni na kutekeleza Mpango huu, unaoonesha dhamira ya dhati ya kuwekeza katika kuandaa kizazi cha wataalam mahiri katika Nyanja za Akili Unde, Sayansī ya Pata, na ulinzi wa mtandao na maeneo mengine katika fani hizo.

Vijana 50 wamepata fursa hiyo ya kufadhiliwa kusoma katīka vyuo mahirī duniani, huu ni mwanzo na kadri tunavyoendelea tunaamini idadi itaongezeka

Shime kwa wazazi,walimu walezi na jamii kuunga mkono juhudi za Serīkali kwa kuhamasisha vijana kujiunga na masomo ya sayansi, kujifunza kwa bidii na kutumia kīkamilifu fursa zilizopo za ufadhili ili wakihitīmu waweze kuchangia katika ustawi na maendeleo ya Taifa.






BODI YA UHARIRI

Sylvia Lupembe
*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Lucas Haule
Fradius Mugoa
Elizabeth Marwa
Dionice Lukweme
Veronica Chitunda
Nazareth Mwakabuta
Suzan Magobeko -SUA

**Mawasiliano:**
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533

**Jarida hili linatolewa na**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Walimu ni nguzo >

# Walimu ni Msingi wa Maendeleoya Taifa - Mhe. Majaliwa



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majliwa Majaliwa amesema walimu ni nguzo ya maendeleo ya taifa. Ameeleza kuwa wanalea kizazi chenye maarifa na ujuzi. Hivyo, mchango wao ni muhimu kwa ustawi wa jamii na uchumi.

Akizungumza Oktoba 03, 2025 mkoani Geita katika maadhimisho ya Siku ya Mwalimu Duniani, Mhe. Majaliwa amesisitiza kuwa mafanikio ya kijamii, kiuchumi na kielimu huanzia darasani kupitia juhudi za walimu. Bila walimu, hakuna taaluma, hakuna viongozi wa kesho, wala taifa imara.



Katika Maadhimisho hayo, ameielekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuweka mifumo ya mafunzo kazini kwa walimu ili waendane na mabadiliko ya teknolojia. Pia amezitaka Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Utumishi kuhakikisha msawazo wa walimu ndani ya mikoa unafanyika ipasavyo

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Prof. Carolyne Nombo, amesema Serikali inaendelea kusimamia Sera ya Elimu, sambamba na kutekeleza mafunzo ya ualimu tarajali na endelevu, na kuboresha miundombinu ya shule kwa walimu kazini.

Amesema kuwa, kupitia mpango wa MEWAKA, walimu wamepata mafunzo bora, yanayohusu mitaala, sayansi, hisabati na TEHAMA. Mafunzo hayo yameongeza umahiri na ufanisi kazini, ikiwemo usawa wa kijinsia na ujumuishi wa wanafunzi.

Prof. Nombo amesema Serikali imeandaa mkakati maalum, kuboresha mazingira ya kazi na maslahi ya walimu. Programu ya Leaders in Teaching imeanzishwa rasmi, ikilenga mbinu za ufundishaji na mafunzo ya ujasiriamali.

Katibu Mkuu Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) Mkoa wa Geita Pauline Ntinda ameipongeza Serikali, na kwamba katika kipindi cha mwaka 2021-25, Mkoa huo umepokea takriban Sh. Bilioni 20 kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya shule, ikijumuisha madarasa 134, nyumba za walimu 103, matundu ya vyoo 332, maabara, maktaba na vifaa mbalimbali vya kujifunzia.

Ameongeza kuwa Serikali imetoa kibali cha upandishaji madaraja kwa walimu 823 na kubadilisha miundo ya utumishi kwa walimu 737 ndani ya mwaka wa fedha 2024/2025. Walimu wa kujitolea 604 wanaolipwa kupitia mradi wa GPE-TSP wamepangwa katika shule za pembezoni, sambamba na ujenzi wa nyumba za walimu. Ajira mpya zimeendelea kutolewa kila mwaka, ambapo walimu 607 waliagizwa mkoani Geita mwaka 2023/2024, na walimu 770 wamepangwa kwa mwaka wa fedha 2024.

Wataalamu wa Nyuklia >

# Tanzania Yaongeza Kasi ya Maandalizi ya Wataalamu wa Nyuklia



Katika kuhakikisha usalama na uendelevu wa matumizi ya teknolojia ya nyuklia, Tanzania imeanza kuandaa rasilimali watu wa Sayansi na Teknolojia ya Nyuklia katika vyuo vya ndani na nje ya nchi Ili kujenga uwezo wa kitaifa na kupunguza utegemezi wa wataalamu kutoka nje ya nchi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, ameeleza hayo Vienna, Austria 17 Septemba 2025 wakati wa kikao maalum na Mkurugenzi wa Divisheni ya Afrika wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA), Dkt. Gashaw Gebeyehu Wolde, kando ya Mkutano Mkuu wa 69 wa IAEA.

Katika kikao hicho, viongozi hao wamejadili maendeleo ya matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia katika sekta za Afya, Kilimo, Maji na Nishati, sambamba na maandalizi ya wataalamu wa ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya nyuklia.

Prof. Nombo amesema kuwa ushirikiano kati ya Tanzania na IAEA umeleta tija kubwa katika sekta ya afya kupitia matibabu ya saratani kwa mionzi, katika kilimo kupitia tafiti za mbegu bora, na katika maandalizi ya matumizi ya nishati safi ya nyuklia.

Dkt. Gashaw Gebeyehu Wolde amepongeza juhudi za Tanzania na kubainisha kuwa ni mshirika muhimu wa IAEA katika ukanda wa Afrika. Ameahidi kuendeleza ushirikiano wa karibu katika miradi ya nyuklia na kuongeza fursa za mafunzo kwa wataalamu wa sekta ya sayansi na teknolojia ya nyuklia, hususan katika vifaa tiba.

Prof. Nombo anaongoza ujumbe wa Tanzania katika Mkutano wa 69 wa IAEA unaoendelea Vienna, Austria.

Prof. Nombo anaongoza ujumbe wa Tanzania katika Mkutano wa 69 wa IAEA unaoendelea Vienna, Austria.







*Serikali imekabidhiwa rasmi majengo ya Shule ya Sekondari mpya Dkt. Samia iliyopo Iyumbu jijini Dodoma, ambayo imegharimu Shilingi bilioni 17.8.*

# Shule ya Sekondari ya Dkt. Samia Dodoma yakamilika na Kukabidhiwa Rasmi

Serikali imekabidhiwa rasmi majengo ya Shule ya Sekondari mpya Dkt. Samia iliyopo Iyumbu jijini Dodoma, ambayo imegharimu Shilingi bilioni 17.8.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Septemba 26, 2025 jijini Dodoma, Mkurugenzi Msaidizi wa Utawala na Rasilimali Watu katika Wizara hiyo Ndug. Fredrick Kayombo, amesema kuwa amekagua majengo yote na kwamba ameridhishwa na kazi iliyofanyika kuwa ni ya ubora na viwango

"Tunaipongeza Serikali chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uwekezaji mkubwa katika Shule hii ya mfano, iliyoyosheheni miundombinu bora na ya kisasa. Ni wajibu wa watendaji kusimamia kikamilifu miundombinu ya shule kwa kuzingatia thamani kubwa ya fedha iliyowekezwa," Amesema Kayombo.

Kayombo amewahimiza wanafunzi wa shule hiyo kusoma kwa bidii ili waweze kufaulu, kuiheshimisha shule yao, na kulinda hadhi yake.

Meneja Ujenzi wa Kanda ya Magharibi wa SUMA JKT CC, Kanali Saul Chimwaga amesema ujenzi huo umezingatia viwango vya juu vya ubora, teknolojia na mifumo ya kisasa ikiwemo ya kuzima moto, ulinzi kwa kutumia kamera za CCTV na matumizi ya biogas.

Meneja wa Mradi huo kutoka kampuni ya Ushauri wa Kitaalam Chuo Kikuu Ardhi (ABECC) Dkt. Kimata Malekela, amesema mradi huo unajumuisha jengo la utawala, madarasa, maabara, ofisi za walimu, ofisi, mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 na nyumba 12 za walimu zinazoweza kuchukua walimu 21.

Mkuu wa shule hiyo, Leticia Singo, ameishukuru Serikali kwa kujenga shule bora yenye usajili kamili kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita. Shule hiyo ina wanafunzi 533 wa kidato cha kwanza, tano na sita, na inapokea wanafunzi wa jinsia zote, wakiwemo wenye mahitaji maalum.

Ameeleza kuwa shule hiyo ni jumuishi, ina miundombinu rafiki, mfumo wa biogas kwa shughuli za upishi na uchujaji wa maji taka kwa matumizi ya bustani.

Pia katika shule hiyo kuna darasa janja linalowawezesha wanafunzi kujifunza kupitia vituo vilivyounganishwa kitaifa la katika mfumo wa TEHAMA.

Samia Scholarship >

# 50 WANUFAIKA SAMIA SCHOLARSHIP EXTENDED DS/AI+



Serikali ya Tanzania imeendelea kuonesha dhamira ya kuwezesha vijana wa Kitanzania kupata elimu ya juu katika fani za Sayansi ya Data, Akili Unde na Sayansi Shirikishi kupitia mpango wa Samia Scholarship Extended DS/AI+.

Katika kikao maalum kilichofanyika Septemba 28,2025 katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST), Arusha, Viongozi wa Wizara na Kamati inayoratibu mpango huo wamefanya tathmini ya awali ya maandalizi na maendeleo ya wanufaika walipo katika Kambi Maalum ya Maarifa.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Daniel Mushi amesema Serikali itahakikisha wanufaika wanapata elimu bora kuijenga Tanzania yenye rasilimali watu wenye ujuzi katika Sayansi na Teknolojia sambamba na kukuza uwezo wa taifa kushiriki kikamilifu katika mapinduzi ya nne ya viwanda na uchumi wa kidijitali.

Makamu Mkuu wa Taasisi ya NM-AIST, Prof. Maulilio amesema Taasisi hiyo inaendelea kushirikiana kwa karibu na Wizara kuhakikisha wanufaika wanapata maarifa ya kiwango cha juu na mafunzo ya vitendo kuwawezesha kuwa tayari kuingia katika Vyuo Vikuu Mahiri Duniani.

Wakizungumza kuhusu fursa ya ufadhili huo, Simon Simon na Malaika Frolence wameeleza kuwa kupitia mpango wa Samia Scholarship Extended (DS/AI+), malengo yao yamepata mwelekeo thabiti. Wamesisitiza kuwa wataitumia kikamilifu fursa hiyo adhimu kwa manufaa yao binafsi na kwa maendeleo ya taifa kwa ujumla.



Mageuzi ya Elimu Nchini >

# Uongozi Imara ni Msingi wa Utekelezaji wa Mageuzi ya Elimu Nchini - Dkt. Omari





Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Hussein Omar, amezitaka Taasisi na Mashirika mbalimbali ya elimu kuimarisha usimamizi na uongozi wa elimu ili kuwezesha kikamilifu utekelezaji wa sera ya elimu na Mafunzo ya 2014 Toleo la 2023.

Dkt. Omari ametoa rai hiyo Oktoba 3, 2025 mkoani Morogoro akizundua Jukwaa la Kitaaluma la Wadau wa Uongozi na Usimamizi wa Elimu Nchini, lililoandaliwa na Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM), ambapo amesema jukwaa hilo litaisaidia Serikali na wadau kuwa na sauti moja, kurahisisha uratibu na kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali katika sekta ya elimu.

**“Kupitia jukwaa hili, tutajua taasisi ipi inafanya nini na wapi, jambo litakalosaidia kuunganisha jitihada za wadau na kuleta matokeo chanya katika elimu,”** amesema Dkt. Omar.

Makamu Mkuu wa Chuo ADEM, Dkt. Emmanuel Mollel, amesema Jukwaa hiilo ni fursa ya kujenga mshikamano kati ya taasisi zinazoshughulika na uongozi wa elimu na elimu kqa ujumla, kushirikiana katika tafiti na kubadilishana utaalamu.

“Tunashukuru kupata nafasi ya kukukutana na wadau wanaofanya kazi zinazofanana katika eneo hili la elimu nchinj. Hii itarahisisha kushirikiana katika matumizi ya rasilimali na kuwa na mwelekeo mmoja ili kufukia malengo mapana ya maendeleo ya Elimu Kitaifa,” ameeleza Dkt. Mollel.

Naye, Kiongozi wa Mradi wa Shule Bora, Virginie Briand, amesema kuwa mradi huo unachangia kuwezesha mafunzo ya kwa viongozi wa shule ili kuwajengea uwezo wa kupanga na kuongoza kimkakati na kukuza utamaduni bora wa kujifunza.



Bajeti Sekta ya Elimu >



# Asilimia 20 ya Bajeti Kuu Hutengwa kwaajili ya Sekta ya Elimu

Naibu Waziri Mkuu ambaye pia ni Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, amesema Serikali imeendelea kuipa kipaumbele sekta ya elimu kwa kutenga takribani asilimia 20 ya Bajeti Kuu kila mwaka kwa ajili ya sekta hiyo.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano wa wadau wa elimu ulioandaliwa na Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET) jijini Dar es Salaam Septemba 24,2025 Dk. Biteko amesema hatua hiyo imeifanya Tanzania kuwa mfano wa kuigwa barani Afrika.

Amesema kuwa Serikali inaendelea kujenga mfumo thabiti wa elimu ya kidijitali na kuongeza matumizi ya rasilimali za ndani ili kuimarisha elimu kwa ajili ya sasa na kwa vizazi vijavyo.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo amesema maboresho makubwa yanayoendelea katika sekta ya elimu yanahitaji uwekezaji wa kutosha wa rasilimali, hivyo Serikali imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu ili kuhakikisha rasilimali muhimu zinapatikana kwa ajili ya kuendeleza sekta hiyo.

Aidha, Prof. Nombo amebainisha kuwa Serikali inaendelea kuwekeza katika kuimarisha mifumo ya utoaji elimu pamoja na kuongeza rasilimali fedha. Hata hivyo, amekiri kuwa bado kuna uhitaji wa rasilimali za kifedha, kitaalamu na kitaaluma ili kufikia malengo kusudiwa.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa TEN/MET, Bi. Martha Makala ameipongeza Serikali kwa kufanya mageuzi ya Kisera, mitaala na uboreshaji wa miundombinu ya shule na ongezeko la walimu, akisema hatua hizo ni msingi wa kufanikisha elimu bora na jumuishi nchini. amesema mtandao huo utaendelea kushirikiana na wadau katika kuimarisha mifumo ya elimu.



Elimu ya Watu Wazima >

# Tanzania yajivunia Mafanikio ya Elimu ya Watu Wazima

## ■ *Zaidi ya wasichana 13,000 wanufaika.*

Serikali ya Tanzania inajivunia kutekeleza miradi mbalimbali kwa mafanikio ikiwemo, mradi wa elimu ya Sekondari Nje ya Mfumo Rasmi, ambapo katika mwaka wa masomo 2025 wanafunzi wapatao 18,886 wavulana 8,648 Wasichana 10,239 wamedahiliwa.

Hayo yameelezwa na Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mhe. Mwanamvua Mrindoko katika Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kisomo Kimataifa na Juma la Elimu ya Watu Wazima Septemba 19, 2025, akimwakilisha Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa.

Mhe. Mrindoko ameongeza kuwa mkakati wa kuwarejesha shuleni Wanafunzi waliopata mdondoko kwa sababu mbalimbali, ambapo zaidi ya Wasichana 13,000 wamenufaika na mpango huo.

Aidha, amebainisha kuwa Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana walio Nje ya Shule (IPOSA) umewanufaisha vijana 12,000, wakiwemo wavulana 5,406 na wasichana 6,594 kwa mafunzo ya muda mrefu. Wanufaika wa mafunzo ya muda mfupi ni 30,183.

"Nimefurahi kusikia miongozo ya program ya Mpango wa Uwiano ya Elimu ha Watu Wazima na Jamii (MUKEJA) imezinduliwa, kwani itasaidia kupunguza idadi ya Watu Wazima wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu" Alisema Mhe. Mrindoka.

Ameipongeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kutekeleza Kwa ufanisi miradi na program za Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Daniel Mushi amesema kuwa Maadhimisho yametoa fursa kwa wadau kujadili mada muhimu kama teknolojia katika elimu, malezi bora, na ujenzi wa stadi kwa vijana. Maadhimisho hayo yalihusisha maonesho, kongamano la kitaifa na kikao kazi




cha Maafisa Elimu kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Mkuu wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW), Prof. Phillipo Sanga, amesema kuwa Taasisi hiyo imejipanga kuongoza kwa ubunifu na dira pana katika kupanua wigo wa fursa za Elimu Msingi Nje ya Mfumo Rasmi nchini.

"Tutaongeza wigo wa kuwafikia Watanzania wote, hususan makundi yaliyoko pembezoni ambayo kwa muda mrefu hayajapata huduma ya elimu stahiki," amesisitiza Prof. Sanga.



Teknolojia >

# Teknolojia ni Nyenzo ya Kuimarisha Elimu ya Watu Wazima na Elimu nje ya Mfumo Rasmi




Mkurugenzi wa Uthibiti Ubora wa Shule Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ephraim Simbeye, amewataka Maafisa Elimu nchini kutumia kikamilifu teknolojia katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku katika utoaji wa elimu bora.

kutekeleza majukumu yao ya kila siku katika utoaji wa elimu bora.

Ametoa rai hiyo Septemba 18, 2025, mkoani Katavi akizungumza katika Kongamano la Juma la Elimu ya Watu Wazima, ambapo amesisitiza kuwa Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya ndio wasimamizi na watekelezaji wa miongozo ya mitaala ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi.

Aidha, ameeleza kuwa Serikali inaendelea kuweka mikakati kabambe ili kupandisha kiwango cha elimu ya mfumo huo, ikiwa ni pamoja na kutokomeza tatizo la kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Watu Wazima kutoka Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mwalimu Ernest Hinju, amesema kuwa kongamano hilo limewaleta pamoja zaidi ya Maafisa Elimu 800 kutoka mikoa yote ya Tanzania, kwa lengo la kujadiliana juu ya njia bora za kuboresha elimu ya watu wazima na kuhakikisha elimu hiyo inakuwa jumuishi, endelevu na yenye tija kwa maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Akikabidhi miongozo ya Programu ya Mpango wa Uwiano kati ya Elimu na Jamii (MUKEJA) iliyotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili, Mkurugenzi wa Shirika la Kimataifa la DVV, Frauke Heinze, amesema wanajivunia kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kuimarisha elimu ya mfumo huo na kwamba elimu ni msingi wa mabadiliko chanya ya kijamii na kiuchumi, na teknolojia ni daraja muhimu kufikia malengo hayo.



Ufadhili >

# Mpango wa MO-KRRY SCHOLARSHIP Wazinduliwa Kuongeza Wataalamu Katika Sekta ya Kilimo na Chakula

## ■ 40 Wanufaika na Ufadhili

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, amesema kuwa ushirikiano ulioanzishwa kati ya Taasisi ya Mo Dewji, Kampuni ya Kerry Group, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) utasaidia kuwaunganisha vijana na viwanda wapate ujuzi.



Prof. Nombo amesema hayo Septemba 25, 2025, jijini Dar es Salaam katika uzinduzi wa Mpango wa Ufadhili wa Mo-Krry Scholarship. Alieleza kuwa ingawa wahitimu wanapata maarifa ya kitaaluma vyuoni, mazingira ya viwanda na teknolojia hubadilika kwa kasi, hivyo kuna umuhimu wa kuwapa vijana fursa ya kujifunza kwa vitendo.

Mpango huu unalenga kuwajengea uwezo wahitimu wa masomo ya Sayansi ya Chakula na Kilimo kutoka vyuo mbalimbali nchini. Kupitia ufadhili huu, wahitimu wataanza kwa mafunzo ya nadharia katika UDSM na SUA kwa kipindi cha miezi minne, wakijifunza mbinu za kisasa na maarifa ya kitaalamu yanayohusiana na sekta ya kilimo na chakula.



Baada ya kukamilisha mafunzo ya darasani, washiriki wa mpango huu watapelekwa katika viwanda vya Mo Dewji kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Hatua hii inalenga kuwapa uzoefu wa moja kwa moja katika mazingira ya kazi, ili kuongeza ujuzi na kuwaandaa kwa ajira au ujasiriamali katika sekta husika.

Mwaka huu jumla ya wanafunzi 40 watanufaika na mpango huo, ambapo Tanzania inatumika kama nchi ya majaribio. Aidha baada ya tathmini ya awali, Mo-Krry Scholarship inatarajiwa kutekelezwa katika nchi nyingine za Afrika Mashariki, ikiwa ni hatua muhimu katika kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kuwezesha vijana wa Afrika kuchangia kikamilifu katika maendeleo endelevu ya barani humo.

Mradi wa HEET >

# Kampasi Mpya Zinazojengwa Chachu ya Mabadiliko ya Kiuchumi katika Jamii.

Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, ikiwemo Tanzania, zinaendelea kukabiliana na vikwazo vya maendeleo endelevu vinavyohusisha changamoto za kiuchumi, kimazingira na kijamii. Changamoto hizo ziinatokana na sababu mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya tabianchi, ukosefu wa usawa katika elimu, na upungufu wa rasilimali muhimu.

Aidha, katika kushughulikia changamoto hizo, vyuo vikuu vimekuwa na mchango mkubwa wa kutoa elimu na kufanya utafiti katika nyanja mbalimbali ili kuimarisha huduma bora za kijamii na kuchochea ubunifu wa na maendeleo ya kiuchumi.

Nchini Tanzania, Taasisi za elimu ya juu zina jukumu la kusimamia ufundishaji, utafiti na huduma kwa jamii, jambo linalowapa nafasi ya kipekee ya kubadilisha maisha ya wananchi walioko jirani na vyuo hivyo.

Tangu mwaka 2021, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatekeleza Mradi wa Mageuzi ya Elimu ya Juu kwa Maendeleo ya Uchumi (HEET), ambao ni mpango mkubwa unaolenga kupanua upatikanaji wa elimu ya juu na kuchochea maendeleo.





Kupitia mradi wa HEET, Taasisi 19 za Elimu ya juu zinanufaika, huku kampasi mpya 16 zikianzishwa katika mikoa 15. Na hadi sasa yapata asilimia 98% ya wakazi wanaufahamu vizuri Mradi huo, Kadri Mradi wa HEET unavyoendelea kutekelezwa, mafanikio ya muda mrefu yataonekana si kwa idadi ya wahitimu tu, bali katika fursa mpya zinazojitokeza kwa wananchi wanaoishi karibu na taasisi hizo zinzazojengwa.

Ujenzi wa Kampasi hizo mpya ambazo husaidia wanafunzi, walimu na wafanyakazi, hali inayoongeza mahitaji ya makazi, chakula na huduma nyingine zinazochochea biashara za ndani. Ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya vyuo hivyo vimezalisha ajira mbalimbali za muda na za kudumu na kuongeza vyanzo vipya vya mapato kwa wakazi wa maeneo husika.

Aidha kipatao cha wakazi jirani na kampasi zinazojengwa kimeanza kuongezeka zaidi, tangu kuanzishwa kwa ujenzi wa kampasi hizo, riporti inaonyesha wastani wa kipato cha TZS 100,000/= mpaka 150,000/= kwa mwezi kwa kila kaya ikijumiisha wanawake kwa wanaume. Pia ripoti inaendelea kueleza asilimia 15% ya kaya kupata mapato kutokana na shughuli wanazofanya kwenye kampasi hizo ikiwemo biashara, kazi zisizorasmi na kukodisha nyumba.

Ingawa faida hazijafikia kila kaya, ujenzi wa kampasi umetoa ajira, mapato, na fursa mpya za biashara, huku changamoto za usawa wa kijinsia na ujumuishaji wa watu wenye ulemavu zikiwa bado zinahitaji kushughulikiwa.

Licha ya uchumi wa wananchi kukua, vyuo hivyo pia vinaboresha tamaduni za jamii kwa kuandaa mihadhara ya umma, matukio ya kitamaduni na shughuli za utafiti. Pia, huchochea maendeleo ya miundombinu kama vile uboreshaji wa barabara na usafiri wa umma, jambo linalochangia maendeleo ya jumla ya jamii.

Teknolojia ya Mbao >

# SUA Yaimarisha Mafunzo kwa Vitendo kwa Wataalamu wa Teknolojia ya Mbao

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimeendelea kuthibitisha ubora wake katika kutoa elimu yenye tija kwa vitendo, kwa kuwawezesha wanafunzi wa Shahada ya Teknolojia ya Mbao na Uongezaji Thamani kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiwanda cha kisasa cha samani kilichopo Kampasi ya Solomon Mahlangu, Morogoro.



Kupitia mafunzo hayo ya vitendo, wanafunzi wanapata fursa ya kujifunza mbinu za kisasa za utengenezaji wa samani, kuanzia hatua ya kukausha mbao kwenye tanuri maalum hadi kutengeneza meza, viti na makabati, sambamba na kutumia mashine za kisasa zinazopatikana kiwandani hapo. Mafunzo haya yanawaandaa sio tu kama wahitimu wa taaluma, bali kama wabunifu na wajasiriamali watakaochangia katika maendeleo ya viwanda na ajira nchini.

Vivian Gwambo, mmoja wa wanafunzi wanaoshiriki mafunzo hayo, amesema: "Kujifunza kwa vitendo kunatupa ujasiri wa kutumia ujuzi tuliojifunza darasani. Kwa sasa tunauona uhalisia wa kile tulichokuwa tunasoma kwenye vitabu na hii inatupa nguvu ya kujua tunaweza kufanya makubwa zaidi kwenye soko la ajira."



Naye Grayson Godfrey ameongeza kuwa mafunzo hayo yamewapa uelewa mpana na ari ya kujenga ubunifu na ubora katika kazi zao za kitaaluma.

Kwa kuweka mkazo kwenye "kujifunza kwa vitendo," SUA inaendelea kuwa kitovu cha kuzalisha wataalamu wabobezi, wabunifu na viongozi wa kesho watakaochangia kwa kiwango kikubwa katika sekta ya viwanda na maendeleo ya taifa.

# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

---

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

---

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET),**
S.L.P 17007, DODOMA.
Simu: +255 26 2323 121 / 0733 77 77 51
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi,
Muhimbili (MUHAS),
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

---

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius
Kambarage Nyerere,
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

---

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
**27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,**
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

---

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

---

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

---

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz

## - KAZI IENDELEE -